



ISSN 0856 - 0323

MWAKA WA 98

17 Machi, 2017

TOLEO NA. 11

# GAZETI

BEI SH. 1,000/=

LA

DAR ES SALAAM

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na  
Kuandikishwa Posta kama Gazeti

## YALIYOMO

Taarifa ya Kawaida Uk.  
Uchaguzi wa Wajumbe wa Tanzania  
Katika Bunge la Afrika Mashariki..... Na.376 1/5

Taarifa ya Kawaida Uk.  
The East African Legislative Assembly  
Election..... Na.376 1/5

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 376

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

TANGAZO

UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TANZANIA KATIKA  
BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

[Chini ya Kanuni ya 12, Kifungu cha 4(1) na 8 cha  
Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge,  
Toleo la Januari, 2016]

**TAARIFA** inatolewa kwa watu wote kwamba,  
**Uchaguzi** wa wajumbe tisa watakaoiwakilisha Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki  
utafanyika wakati wa Mkutano wa Saba wa Bunge, katika  
Ukumbi wa Bunge Dodoma unaotarajiwa kuanza tarehe 4  
Aprili, 2017.

Kwa ajili hiyo basi, Mimi Dr. Thomas D. Kashililah  
nikiwa Msimamizi wa Uchaguzi huo, **ninatoa Taarifa na  
kutangaza kwamba, tarehe 30 Machi, 2017 saa kumi  
(10.00) Jioni, kuwa ndiyo siku ya Uteuzi; na kwamba,  
tarehe 4 Aprili, 2017, saa tano (5.00) Asubuhi, mara au  
mapema baada ya Kipindi cha Maswali, wakati Bunge  
likiwa linaendelea na Shughuli zake, kuwa siku ya  
uchaguzi.**

Pamoja na **TANGAZO** hili, masharti kuhusu uteuzi  
wa Wagombea wa uchaguzi huo yameambatishwa kwa  
ajili ya rejea na uzingatiwaji.

Dodoma,  
15 Machi, 2017

DR. THOMAS D. KASHILILAH,  
Msimamizi wa Uchaguzi

Matangazo yahasuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa  
kwa umma yaweza kuchapishwa katika Gazeti. Yapelekwe kwa **Mhariri, Ofisi ya Rais –Menejimenti ya Utumishi wa  
Umma, S.L.P. 2483, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 2118531/4.** Kabla ya *Jumamosi ya kila Juma.*

**DONDOO ZA KANUNI ZA UTARATIBU WA  
UTEUZI WA WAGOMBEA WA UCHAGUZI WA  
NAFASI ZA UBUNGE KATIKA BUNGE LA AFRIKA  
MASHARIKI**

1. Wabunge tisa watakwaiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, watachaguliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, si kutoka miongoni mwa Wabunge wa Bunge hilo, bali kutoka miongoni mwa watu wanaowakilisha, kwa kadri inavyowezekana, Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, maoni mbalimbali, jinsia pamoja na makundi mengine yenye maslahi maalum, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

2.-(1) Mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kugombea na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki endapo mtu huyo:-

- (a) Ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (b) Anazo sifa za kustahili kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
- (c) Si Waziri katika Serikali;
- (d) Si mtumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (e) Anao uzoefu uliothibitishwa au moyo wa kupenda kuimarisha na kuendeleza malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa matakwa na masharti ya Kanuni ndogo ya (1) (a) na (b), kila Chama cha Siasa kinachokusudia kuteua na kusimamisha Wagombea wake katika Uchaguzi kinatakiwa, siku tano (5) kabla ya siku ya uteuzi, kuwasilisha majina ya wagombea hao katika Idara ya Uhamiaji, na pia katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa ajili ya uthibitisho wa uraia na sifa za wagombea hao, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Kifungu cha 36 cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343.

3. Idara ya Uhamiaji na Tume ya Taifa ya Uchaguzi itathibitisha uraia na sifa za kuwa mgombea kuhusiana na majina ya Wagombea yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 2(2), na kuwasilisha taarifa yake kwa Msimamizi wa Uchaguzi (Katibu wa Bunge) na pia kwa Vyama husika vya Siasa, siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi.

4. Kwa madhumuni ya Uchaguzi huu, "siku ya uteuzi" maana yake ni siku ambayo Msimamizi wa

Uchaguzi, kwa Tangazo katika Gazeti la Serikali, ameipanga kuwa ndiyo siku ya mwisho ya kuwasilisha na kupokea nyaraka za uteuzi wa Wagombea; na "siku ya uchaguzi" maana yake ni siku ambapo Uchaguzi wa kuwachagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki utafanyika.

5. Ili mtu atambulike kuwa ameteuliwa kihalali kuwa Mgombea wa uchaguzi, ni sharti awe ameteuliwa na Chama cha Siasa kinachompendekeza, kwa utaratibu ulio wazi na wa kidemokrasia, na kwa ajili hiyo, nyaraka za uteuzi zitawekwa saini na Mgombea na pia na Katibu Mkuu wa Chama hicho, na zitakuwa na taarifa zifuatazo:-

- (a) Jina la Mgombea, anuani yake, elimu yake na kazi yake; na
- (b) Uthibitisho wa Mgombea kwamba yupo tayari na anazo sifa zinazostahili kuwa Mgombea katika Uchaguzi huo.

6.(1) Mgombea mwenyewe au kiongozi wa Chama cha Siasa kilichomteua atawasilisha nyaraka za uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi (Katibu wa Bunge), Ofisini kwake, Dodoma, kabla ya saa kumi Jioni (10.00) ya siku ya uteuzi, zikiambatana pia na nyaraka zifuatazo:-

- (a) Uthibitisho wa uraia wa mgombea, uliotolewa na Idara ya Uhamiaji;
- (b) Wasifu wa Mgombea, uliowekwa saini na Mgombea mwenyewe, itakayomwezesha Msimamizi wa Uchaguzi kuamua iwapo mgombea anao au hana uzoefu unaohitajika au moyo wa kupenda kuimarisha na kuendeleza malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 50(2) (e) ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (c) Dondoo ya muhtasari wa Mkutano wa Chama ulioidhinisha uteuzi wa mwisho wa Mgombea, iliyowekwa saini na Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano huo, itakayomwezesha Msimamizi wa Uchaguzi kuamua iwapo Mkutano huo wa Chama ulifanyika au haukufanyika kwa utaratibu ulio uwazi na wa kidemokrasia, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

(2) Chama chochote chenye haki ya kusimamisha Wagombea, isipokuwa Chama Tawala ambacho hakitawasilisha majina ya Wagombea kwa Kundi C, kinaweza kuwasilisha majina ya Wagombea watatu kwa kila nafasi wazi katika makundi yafuatayo:-

Kundi A: Wagombea Wanawake;

Kundi B: Wagombea wa Zanzibar;

Kundi C: Wagombea wa Vyama vya Upinzani; na

Kundi D: Wagombea wa Tanzania Bara.

7. Mgombea mwenyewe au kiongozi wa Chama cha Siasa kilichomteua, wakati wa kuwasilisha nyaraka za uteuzi, atalipia kiasi cha shilingi elfu hamsini ambazo hazitarejeshwa, kwa ajili ya gharama za Uchaguzi.

8. Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kuzikataa nyaraka za uteuzi wa Mgombea iwapo nyaraka hizo zitaonyesha wazi kuwa Mgombea huyo hana sifa za kuwa Mgombea wa Uchaguzi; na kwa sababu hiyo, Msimamizi wa Uchaguzi atazikataa nyaraka hizo za uteuzi.

9.- (1) Mgombea anaweza kuondoa jina lake na kujitoa katika Uchaguzi, kwa kutoa taarifa ya maandishi aliyoitia saini na kuiwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi, na nakala yake kuipeleka kwa Katibu wa Chama cha Siasa kilichomteua, kabla ya saa kumi (10.00) jioni, siku moja kabla ya siku ya uteuzi, ambapo baada ya hapo, kujitoa katika uchaguzi hakutaruhusiwa.

(2) Endapo Mgombea atafariki baada ya saa kumi (10.00) jioni ya siku ya uteuzi, lakini kabla ya siku ya uchaguzi, mchakato wa uchaguzi utaendelea.

10.- (1) Mgombea anaweza kujitambulisha kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndio wapiga kura wa Uchaguzi na kuomba kupigi wa kura hata kabla ya siku ya uteuzi na anaweza kuendelea kufanya hivyo baada ya siku ya uteuzi.

(2) Kabla ya kura hazijaanza kupigwa katika siku ya Uchaguzi, kila Mgombea ataruhusiwa kuingia katika Ukumbi wa Bunge, wakati Bunge likiwa linaendelea na shughuli zake, kwa ajili ya kujieleza mbele ya Wabunge ambao ndio wapiga kura, kwa lugha ya Kingereza na kujibu maswali atakayoulizwa na Wabunge, kama yatakuwepo, kwa muda atakaoruhusiwa na Spika kwa ajili hiyo.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

\_\_\_ PARLIAMENT OF  
TANZANIA

\_\_\_  
**NOTICE**  
\_\_\_

THE EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY  
ELECTION

*[Made under Order 12, rule 4(1) and 8 of the Third  
Schedule of the Parliamentary Standing Orders,  
January, 2016 Edition]*

**NOTICE** is hereby given to the general public that, **Election** of nine members of the United Republic of Tanzania to the East African Legislative Assembly will be held during the Seventh Meeting of Parliament, scheduled to take place in the Parliamentary Debating Chamber at Dodoma from the 4<sup>th</sup> day of April, 2017.

In that respect therefore, I, Dr. Thomas D. KASHILILAH being the Returning Officer for that election, DO HEREBY declare and appoint **four o'clock in the afternoon (4.00 p.m.) of the 30<sup>th</sup> day of March, 2017 to be nomination day and eleven o'clock in the morning (11.00 a.m) of the 4<sup>th</sup> day of April, 2017 after Question time or so soon thereafter, when the National Assembly shall be sitting in ordinary session, to be election day.**

Together with this **NOTICE**, extract of rules of procedure for nomination of candidates for the election are provided for easy reference and compliance.

Dodoma,  
15<sup>th</sup> March, 2017

DR. THOMAS D. KASHILILAH  
*Returning Officer*

**EXTRACT OF RULES OF PROCEDURE FOR  
NOMINATION OF CANDIDATES FOR THE  
ELECTION OF MEMBERS OF THE EAST  
AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY**

1. The nine members who shall represent the United Republic of Tanzania in the East African Legislative Assembly shall be elected by the National Assembly of Tanzania, not from among its members but from among persons who shall represent, as much as it is feasible, the various political parties represented in the National

Assembly, shades of opinion, gender and other special interest groups, in accordance with the Parliamentary Standing Orders, January 2016 Edition.

2.-(1) A person shall be qualified to stand for election to be a member of the East African Legislative Assembly if such person:

- (a) is a citizen of the United Republic of Tanzania;
- (b) is qualified to be elected a member of the National Assembly of Tanzania in accordance with the provisions of Article 67 of the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977;
- (c) is not holding office as a Minister;
- (d) is not an officer in the service of the East African Community; and
- (e) has proven experience or interest in consolidating and furthering the aims and the objective of the East African Community.

(2) For purposes of compliance to the requirements of sub-rule (1) (a) and (b), every political party which intends to nominate its candidates to take part in the election, shall five (5) days before the nomination day, submit the names of its candidates to the Immigration Department and to the National Election Commission respectively, for certification of citizenship and qualification for election, in accordance with the provisions of Article 67 of the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977 and Section 36 of the National Elections Act (Cap. 343).

3. The Immigration Department and the National Election Commission shall certify citizenship and qualification for election in respect of the names of candidates submitted pursuant to the provisions of rule 2(2), and three (3) days before the nomination day, submit its report to the Returning Officer and to the political parties concerned.

4. For purposes of the election, "nomination day" means the day which the Returning Officer by notice published in the *gazette*, has set to be the last day for receiving nomination papers, and "election day" means the day on which the election of members of the East African Legislative Assembly is set to be conducted.

5. In order to be validly nominated as a candidate for the election, a person must be nominated in a transparent and democratic manner by the political party sponsoring him, and for that purpose, the nomination papers shall be signed by the candidate and the Secretary General of the political party nominating him, and shall contain the following:

- (a) The name, address, education qualification and occupation of the candidate; and
- (b) A certificate by the candidate that he is willing and qualified to stand for election.

6.-(1) The candidate or an official of the political party nominating him shall deliver the nomination papers to the Returning Officer at his Office, Dodoma, not later than four o'clock in the afternoon (4.00 p.m.) of the nomination day, accompanied by the following documents:-

- (a) Proof of citizenship of the candidate, issued by the Immigration Department;
- (b) Detailed biographical information of the candidate, signed by the candidate himself, which shall enable the Returning Officer to determine whether or not the candidate has proven experience or interest in consolidating and furthering the aims and objectives of the Community in terms of Article 50(2) (e) of the Treaty; and
- (c) An extract of the nomination proceedings of the party organ which approved the final nomination of the candidate, signed by the Chairman and Secretary of that organ which shall enable the Returning Officer to determine whether or not the relevant political party's proceedings were transparent and democratic in terms of the Political Parties Act.

(2) Any political party which is entitled to sponsor candidates, except for the ruling party which will not submit names of candidates for group C, may submit to the Returning Officer names of three candidates for each vacant seat in the following relevant groups:-

- Group A: Women Candidates;
- Group B: Zanzibar Candidates;
- Group C: Opposition Parties Candidates; and
- Group D: Mainland Candidates.

7. A candidate or an official of the party nominating him shall, at the time of delivering the nomination papers, deposit a non-refundable deposit of fifty thousand shillings to cover for the cost of election expenses.

8. Objection may be made by the Returning Officer to the nomination of a candidate, if it is apparent to him from the contents of the nomination papers that the candidate is not qualified to stand for election; in which case the Returning Officer shall forthwith reject the nomination papers of that candidate.

9.-(1) A candidate may withdraw his candidature by notice in writing, signed and delivered by him to the Returning Officer and a copy to the secretary General of the political party sponsoring him, not later than four o'clock in the afternoon (4.00 p.m.) of the day following nomination day, thereafter no withdrawal shall be accepted.

(2) Where any candidate dies after four o'clock in the afternoon (4.00 p.m.) of the nomination day and before election day, the election process shall continue undisturbed.

10.- (1) A candidate may introduce himself to the members of the National Assembly who are the voters for the election and seek the necessary support even before the nomination day and may continue to do so after nomination day.

(2) Before the votes are casted on the election day, each candidate shall be permitted to appear before the voters, duly assembled in an ordinary sitting of the House and address them in English for such length of time and answer such number of questions, if any, as may be determined by the Speaker for that purpose.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



---

## **UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI**

---

### **TAARIFA KWA UMMA**

KUHUSU

### **MGAWANYO WA MAKUNDI NA IDADI YA WAGOMBEA KATIKA KILA KUNDI**

*(Chini ya Kanuni ya 12 na Kanuni 11(4) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu  
za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

---

- 1.1 Kwa mujibu wa Ibara ya 50 (1) ya Mkataba, Kanuni ya 5(5) na 11(3) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kwa kuzingatia mazingira ya Tanzania uwakilishi wa Wajumbe wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki utakuwa katika makundi yafuatayo:
  - (a) Kundi A: Wanawake;
  - (b) Kundi B: Zanzibar;
  - (c) Kundi C: Upinzani; na
  - (d) Kundi D: Tanzania Bara.
  
- 1.2 Katika uchaguzi wa mwaka huu 2017 mgawanyo wa makundi na upangaji wa idadi ya wagombea katika makundi hayo umezingatia uwiano wa idadi ya Wabunge waliopo Bungeni kwa kila Chama chenye uwakilishi Bungeni.

1.3 Uwiano wa idadi ya Wabunge kwa kila chama kati ya wabunge 391 waliopo Bungeni kwa sasa ni kama ifuatavyo:

- (a) Chama cha Mapinduzi (CCM) Wabunge 275 sawa na 70.33%;
- (b) Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wabunge 72 sawa na 18.41%;
- (c) Chama cha Wananchi-CUF Wabunge 42 sawa na 10.74%;
- (d) Chama cha NCCR- MAGEUZI Mbunge mmoja sawa na 0.25%; na
- (e) Chama cha ACT -Wazalendo Mbunge mmoja sawa na 0.25%.

1.4 Kwa kuzingatia uwiano huo, kila Chama chenye uwakilishi Bungeni kina haki ya kupata viti kwa mchanganuo ufuatao:

- (a) Chama cha Mapinduzi (CCM) chenye wabunge 275 sawa na 70.33% ya wabunge wote kinatakiwa kupata viti sita (6);
- (b) Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) chenye Wabunge 72 sawa na 18.41% ya wabunge wote kinatakiwa kupata viti viwili (2);
- (c) Chama cha Wananchi-CUF chenye wabunge 42 sawa na 10.74% kinatakiwa kupata kiti kimoja (1); na
- (d) Chama cha NCCR- MAGEUZI na Chama cha ACT-Wazalendo vyenye Mbunge mmoja mmoja (1) sawa na 0.25% havitapata kiti kutokana na kuwa na idadi isiyotosheleza (*threshold*) kupata nafasi ya uwakilishi katika Bunge la Afrika Mashariki.

1.5 Kwa muktadha huo, Mheshimiwa Spika kwa mamlaka aliyonayo ameamua idadi ya uwakilishi kwa kila kundi uwe kama ifuatavyo:

- (a) **Kundi A: Wanawake** - Mjumbe mmoja (1) kutoka Chama Cha Mapinduzi(CCM);
- (b) **Kundi B: Zanzibar** - Wajumbe Wawili (2) kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM);
- (c) **Kundi C: Vyama vya Upinzani** – Wajumbe Watatu (3) kulingana na uwiano wa Idadi ya Wabunge wa Upinzani waliopo

Bungeni hivyo, uwakilishi katika Kundi hili utakuwa Wajumbe Wawili kutoka CHADEMA na Mjumbe Mmoja kutoka CUF; na

(d) **Kundi D: Tanzania Bara** – Wajumbe Watatu (3) kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM).

1.6 Hivyo, idadi na uwiano wa Wajumbe wataochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki utakuwa CCM Wajumbe Sita (6), CHADEMA Wajumbe Wawili (2) na CUF Mjumbe Mmoja (1).

Imetolewa na:

Dr. Thomas D. Kashililah  
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**  
15 Machi, 2017